

SEHEMU YA KUMI NA NNE
WAGENI BUNGENI

113.-(1) Spika aweza kutoa ruhusa maalum au ya jumla kwa mwakilishi wa chombo chochote cha habari kuhudhuria vikao vya Bunge katika sehemu ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge iliyotengwa kwa ajili hiyo.

Ruhusa
kwa
Waa-
ndishi
wa
Habari

(2) Ruhusa yoyote itakayotolewa kwa mujibu wa fasili ya (1) yaweza kuwekewa masharti yoyote ambayo Spika ataona yanafaa.

(3) Spika aweza wakati wowote kuondoa ruhusa aliyotoa kwa mwakilishi wa chombo chochote cha habari, iwapo chombo hicho kitatoa taarifa yoyote kuhusu Shughuli za Bunge, ambayo kwa maoni ya Spika, si ya haki, si ya kweli au inapotosha ukweli, au vinginevyo inakiuka Kanuni na taratibu, au haki za Bunge.

(4) Masharti ya Kanuni ya 115 yatatumika kuhusu wawakilishi wa vyombo vyote vya habari, isipokuwa kama Bunge litaamua vinginevyo.

114.-(1) Wageni waweza kuruhusiwa kuingia katika Ukumbi wa Mikutano ya Bunge katika sehemu yoyote ya Ukumbi huo ambayo itatengwa kwa ajili hiyo.

Ruhusa
kwa
Wageni
wengi-
neo

(2) Wakiwa ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge, wageni sharti wakae kimya, na kwa heshima inayostahili, na sharti watoke nje ya Ukumbi huo na mazingira yake endapo Spika atawataka wafanye hivyo.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya fasili (2), wageni yawabidi:-

- (a) Wavae mavazi ya heshima kabla ya kuingia katika Ukumbi wa Mikutano ya Bunge;
- (b) Waingie au watoke Ukumbini kwa staha;
- (c) Wasisome kitabu chochote, gazeti, barua au hati nyingineyo ambayo si Orodha ya Shughuli za Bunge;
- (d) Wasiandike jambo lolote linalozungumzwa, ila tu kama ni mwakilishi wa chombo cha habari;
- (e) Wasizungumze kwa sauti ya juu;
- (f) Wasivute sigara au kiko wakati wowote wakiwa ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge, au mahali popote nje ya Ukumbi huo ambapo kuna mahali pa kukaa wageni.

Mamlaka
ya
kuwao-
ndoa
wageni
Bungeni

115.-(1) Wakati wowote atakapoona yafaa kufanya hivyo, Spika aweza kuamuru wageni watoke nje ya sehemu yoyote ya Ukumbi, na mazingira yake, na aweza kuamuru milango ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge ifungwe.

(2) Endapo, wakati wa kikao chochote, Mbunge atatoa hoja kuwa wageni watoke nje, Spika atalihoji Bunge papo hapo na hoja itaamuliwa bila ya mjadala au mabadiliko yoyote.

(3) Mtumishi yeyote wa Bunge hataruhusiwa kumtoa nje mgeni au kuagiza mgeni atolewe nje endapo Spika ameruhusu mgeni huyo kutumia chombo cha kupigia picha au kunasia sauti katika Ukumbi wa Bunge.